

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA DARASA LA NNE

002

KISWAHILI

MUDA: SAA 2.00

JUMATATU 6 NOVEMBA, 2023 MCHANA

MAELEKEZO KWA MTAHINIWA

- 1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.**
- 2. Jibu maswali YOTE katika kila sehemu.**
- 3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.**
- 4. Majibu YOTE yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.**
- 5. Majibu YOTE yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.**
- 6. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.**

KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
JUMLA		
SAINI YA MHAKIKI		



00742301

Mtihani huu una kurasa 7 zenye maandishi

SEHEMU A: (Alama 20)

IMLA NA UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Sikiliza kwa makini sentensi zitakazosomwa na msimamizi kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi iliyowachwa wazi.

- i. _____
- ii. _____
- iii. _____
- iv. _____
- v. _____

2. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

Bi Ashura ni mkaazi wa Kijiji cha Tupendane. Maisha yake ya kila siku yanategemea kilimo. Bi Ashura hulima mishokishoki, mihaliudi na miti mengine ya matunda. Ameajiri vijana wengi katika shehia yake. Vijana hao hufanya kazi ya kupanda mbegu za miti na kwenda kuuza miche kwa wateja.

Bi Ashura ni hodari kwa kazi ya upandaji wa miti. Siku moja alialikwa na mzee Hemedi, Sheha wa shehia ya Tupendane ili aweze kuwahutubia wakaazi wa kijiji hicho juu ya upandaji na faida za miti. Pia awambie hasara za kutopanda miti. Bi Ashura alianza kwa kusema, "tunza mazingira ili yakutunze! Jangwa ni janga! Tupendane inawapasa kuyajali, kuyatunza na kuyahifadhi mazingira yetu. Miti ni uhai wa maisha yetu. Faida zake ni kupata hewa, mvua ya kutosha, kipato cha ziada, kuni na mkaa. Vilevile tunapata mbao kwa ajili ya kujengea na kutengenezea samani kama vile viti, meza, madawati, makabati, vitanda na stuli."

Sheha naye aliwaeleza umuhimu wa kutunza mazingira. Utunzaji huu utawaepusha na magojwa kama vile malaria, tumbo la kuendesha na homa ya matumbo. Alisisitiza kuwa, kila mmoja awe mlinzi wa

mwengine katika kutunza mazingira. Endapo mtu atakata mti mmoja, basi apande miti mengine mitano ili kuepusha jangwa.

Wanatupendane walisikiliza kwa makini hotuba hiyo. Walipata shauku ya kutaka kuuliza maswali, lakini kutokana na muda kuwa finyu, hawakuweza. Mzee Hemedi aliwaahidi kuwatembelea wakati mwengine ili wapate fursa ya kujua zaidi. Bi Ashura alimalizia kwa kuwambia Wanatupendane "Tukiamua kwa pamoja inawezekana, kata mti panda miti".

MASWALI

a) Bi Ashura anaishi wapi?

b) Taja aina mbili (2) za miti inayolimwa na bi Ashura.

i. _____

ii. _____

c) Andika kazi mbili (2) wanazozifanya vijana walioajiriwa na bi Ashura.

i. _____

ii. _____

d) Kwa nini mzee Hemedi alimualika bi Ashura?

e) Bainisha ujumbe aliutoa bi Ashura mwisho wa mkutano.

SEHEMU B: (Alama 40)
SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA
Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

3. Badilisha sentensi zifuatazo katika hali ya ukanushi.

i. Leo ni siku ya furaha.

ii. Wageni wetu watakuja kesho.

iii. Mimi napenda kusoma vitabu.

iv. Paka ana mkia mrefu.

v. Washindi walipewa zawadi.

4. Taja aina za vivumishi vilivyopigiwa mstari.

i. Mti mrefu umeanguka.

ii. Ni mtoto yupi aliyevunjika mguu?

iii. kitabu changu kimechanika.

iv. Gari sita zimenunuliwa mwaka huu.

v. Baskeli yenyewe ni mbovu.

5. Tumia sentensi tano (5) kuitambulisha familia yako kwa rafiki yako wa karibu.

6. a) Andika tarakimu zifuatazo kwa maneno.

i. 306

ii. 49,252

iii. 127,505

- b) Tafsiri sentensi zifuatazo kwa lugha ya Kiingereza.

i. Mwaka ujao nitakuwa darasa la tano.

ii. Rais wa Zanzibar ni Dk. Hussein Ali Mwinyi.

SEHEMU C: (Alama 20)

FASIHI NA UTAMADUNI

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

7. a) i) Nini maana ya Majigambo?

- ii) Toa mfano mmoja (1) wa Majigambo kuhusu skuli yako.

- b) Taja aina tatu (3) za vyakula vya asili vya mswahili.

i) _____

ii) _____

iii) _____

SEHEMU D: (Alama 20)

UTUNGAJI

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

8. Zakia anashindwa kutunga Insha ya picha. Muelekeze vipengele muhimu vya utungaji wa Insha hiyo.

Nambari ya Mtahiniwa _____

[illegible]

